



# Shughuli za Njoo, Unifuate

Kwa ajili ya jioni ya nyumbani, kujifunza maandiko—au kwa ajili ya burudani tu!

Julai 1-7


## Sanaa ya Mpango wa Furaha

KWA AJILI YA ALMA 17-22

Haruni na Amoni wote wawili walifundisha kuhusu mpango wa furaha wa Baba wa Mbinguni. Wao waliiuta mpango wa ukombazi (ona Alma 18:36-39 na Alma 22). Geuza ukurasa wa 12 ili kutengeneza sanaa yako ya mpango wa furaha.

### Kwa ajili ya watoto wadogo:

Tafuta picha ya mtoto wako alipokuwa mtoto mchanga. Onyesha njia ambazo wamekua tangu walipokuwa watoto wachanga! Kisha zungumza kuhusu uwepo wetu duniani wa kukua kama sehemu ya mpango wa Baba wa Mbinguni.



Julai 8-14

## Vyombo Mikononi mwa Mungu

KWA AJILI YA ALMA 23-29

Amoni alisema kwa kaka zake, "Sisi tumefanya vyombo katika mikono ya Mungu kutimiza kazi hii kubwa" (Alma 26:3). Kusanya vitu unavyoweza kuvitumia kutengeneza muziki. Kisha ufanye midundo na nyimbo. Kama vile tu tunavyotumia vyombo kufanya muziki, Mungu anaweza kututumia sisi kusaidia kujenga Kanisa la Yesu Kristo.

**Kwa watoto wadogo:** Fanya somo la vikwazo rahisi. Fanya mazoezi ya kulipitia! Kisha ondoa vikwazo na ujaribu tena. Elezea jinsi gani mfalme wa Walamani aliondoa vikwazo wakati Amoni na kaka zake walipotaka kufundisha injili katika nchi yake (Alma 23:3).

VIELEZO NA KATY DOCKRILL

Julai 15-21

## Kumbusho la Viti vya Muziki

KWA AJILI YA ALMA 30-31

Alma alifundisha kwamba "vitu vyote vinaonyesha kwamba kuna Mungu" (Alma 30:44). Hiyo inamaanisha kwamba kila kitu Mungu alichokiumba kinatukumbusha juu Yake. Panga viti katika duara kukiwa na viti vya kutosha kwa kila mtu isipokuwa mtu mmoja. Mtu mwininge na apige muziki na kuchagua wakati gani azime. Muziki unapozima, kila mtu anakaa kwenye kiti. Mtu ambaye anakosa kiti anashiriki kitu kimoja ambacho kinawakumbusha juu ya Mungu. Endelea hivyo mpaka kila mmoja amepata zamu ya kushiriki.

### Kwa ajili ya watoto wadogo:

Tembea kuzunguka nyumba ndani au nje. Tafuta vitu ambavyo vinakusaidia kuwa na furaha na kukukumbusha juu ya Baba wa Mbinguni.



Julai 22-28

## Kukuza Ushuhuda Wako

KWA AJILI YA ALMA 32-35

Alma alifundisha kwamba unaposikiliza neno la Mungu na kufanya vitu ili kuonyesha imani yako, ushuhuda wako utakua, kama mti (ona Alma 32:37). Chora vitu unavyoweza kufanya ili kusaidia mti kukua, kama kuupatia maji, na mwangaza wa jua. Kisha chora vitu unavyoweza kufanya ili kusaidia ushuhuda wako kukua, kama kwenda kanisani na kusali.

**Kwa Watoto wadogo:** Imba "Faith" (*Kitabu cha Nyimbo za Watoto*, 96). Wakati unaimbua, fanya vitendo kuonyesha mbegu inakua kubwa na ndefu. Zungumza kuhusu kukuza ushuhuda wako.